

Kukutana kwa Familia: Wakimbizi au watu waliopewa Ulinzi wa Fadhila

Taarifa ifuatayo itakusaidia kukusanya habari na ushahidi mwingi kama iwezekanavyo kabla ya kumwendea mshauri wa kisheria au wakili ili kujadili kukutana kwa familia.

Kama una **Hadhi ya Mkimbizi** au **Ulinzi wa Fadhila** na unataka mshirika wa familia aje na aishi na wewe nchini Uingereza, utahitajika kutoa ushahidi wa zifuatazo:

- Kwamba una hadhi ya ukimbizi. Kwa mfano Hati ya Hadhi yako ya Uhamiaji.
- Kwamba wanahusiana na wewe na waliishi katika familia yako kabla ya wewe kuondoka. Kwa mfano cheti cha ndoa au cha kuzaliwa/kuchukuliwa, picha za harusi au familia.
- Kwamba bado munawasiliana mara kwa mara. Kwa mfano kadi za simu, barua, risiti za hawili ya pesa.

Washirika wa familia yako walio ngambo lazima wadhibitishie kwa Ubalizi wa Uingereza:

- 1) Katika kesi ya mume/mke/ndoa za kiserikali¹
 - Nyinyi wote muna umri wa miaka 21 au zaidi.
- 2) Katika kesi ya mtoto (pamoja na waliochukuliwa)
 - Yeye yuko chini ya umri wa miaka 18 na hajaolewa au anaishi kivyake. (Kama mtoto wako anakaribia umri wa miaka 18, tafadhali uliza ushauri mara moja – lazima uombe kabla ya siku yake ya kuzaliwa ya 18.)
- 3) Katika kesi ya jamaa wengine
 - Kwamba bado wanakutegemea, kwa mfano kwamba unawatumia pesa, au wako peke yao au ni wazee, au ni jamaa wa karibu, na;
 - Kwamba hali yao “inashurutisha na ya huruma”². Hii inamaanisha kwamba wanapitia ugumu na hakuna mtu mwingine wa kuwajali.

Habari zingine muhimu:

- Hati yoyote asili inapaswa kutafsiriwa kwa Kiingereza.
- Kama mshirika wa familia yako ana pasipoti au hati ya kujitambua, itasaidia sana kwa maombi yako.
- Kwa sasa wanaishi katika hali gani? Wanaishi na nani? Ni nani anayewasaidia?

¹ Utambuaji wa Kisheria wa uhusiano wa jinsia moja

² Matini kutoka kwa Kitengo cha Sera cha Ofisi ya Nyumbani kwa IAT, 29 Juni 2004

Ushahidi muhimu ambao unaweza kukusanya ili kuridhisha Sheria hizi

Mahitaji ya Sheria	Mifano ya Ushahidi
Hadhi ya Ukimbizi au Ulinzi wa Fadhila	Hati ya Hadhi yako ya Uhamiaji Hati yako ya Usafiri
Uhusiano/sehemu ya familia	Cheti chako cha ndoa Cheti cha mtoto cha kuzaliwa/kuchukuliwa Picha yako ya harusi au ya familia
Mawasiliano ya Mara kwa mara	Kadi za simu au rekodi Barua Risiti za hawili ya fedha

Ni nani anaweza kusaidia?

Baraza la Wakimbizi la Uskoti halitoi tena huduma ya kukutana kwa familia. Walakini, wakili wako wa kisheria huenda akakusaidia.

Kama huna mmoja au ungetaka kubadilisha wakili wako, tunaweza kukupa majina na anwani za mawakili wa kisheria.

Kama ilivyoandikwa hapo juu, kama unataka kufuatilia suala hili, tafadhali hakikisha kwamba umezingatia mahitaji na ushahidi unaohitajika kabla ya kuomba.



The Scottish Refugee Council 5 Cadogan Square,
(170 Blythswood Court) Glasgow G2 7PH
Ushauri wa bure wa simu: 0800 085 6087
Barua pepe: info@scottishrefugeecouncil.org.uk
Tovuti: www.scottishrefugeecouncil.org.uk
Nambari ya Fadhili Iliosajiliwa: SC008639

